Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA
SHULE YA SEKONDARI PANKUMBI
MTIHANI WA UPIMAJI KIDATO CHA NNE FEBRUARI 2020

021 KISWAHILI

MUDA: SAA 2

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA
1.Mtihani huu una sehemu A,B na C
2.Jibu maswali yote katika sehemu A na B kisha maswali matatu katika sehemu C
3.Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali

SEHEMU A Alama 15

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo;

i. …..Ni misimu ambayo inajulikana katika eneo dogo sana;
a)Misimu zagao b)Misimu ya pekee c) Misimu ya kitarafa d) Misimu pendwa ( )

ii. Ni kiambishi gani kinadokeza njeo kati ya vilivyokolezwa wino?
a)**M**chezo b)Si**ku**mchezea c)Mcheza**ji** d)Wana**tu**chezea ( )

iii. Ni taaluma inayohusiana na utunzi na matumizi ya kamusi
a) Kitomeo b)Kidahizo c)Lugha kienzo d)Leksikografia ( )

iv. ……Ni aina ya sarufi inayoshughulikia mpangilio wa sentensi
a)Sarufi matamshi b)Sarufi maumbo c)Sarufi muundo d)Sarufi maana ( )

v. …Ni maneno yanayotaja tendo lililotendeka, linalotendeka na linalotarajiwa kutendeka
a)Nomino b)Vielelezi c)Vivumishi d)Vitenzi ( )

vi. "*Mtoto anacheza **vizuri***"……**Vizuri –**ni kielelezi cha**;**
a)Sifa b)Namna c)Idadi d)Mahali ( )

vii. Kwa maneno mengine fonolojia tunaweza kuiita……
a)Sarufi muundo b)Sarufi matamshi c)Sarufi muundo d)Sarufi maana ( )

viii. Neno lililotokana na shughuli za utawala enzi za waarabu nchini Tanganyika
a) Sadaka b) Kadhi c) Faida d) Binzali ( )

ix. Kipi si sahihi kati ya hivyo kuhusu asasi za kukuza kiswahili baada ya uhuru wa Tanzania?
a) CHAUKIDU b) TATAKI c) CHAWAKAMA d) CHANETA ( )

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

x. ……..Ni Sauti zinazotamkwa kwa kuzuia mkondo wa hewa kutoka mapafuni kwenda nje kupitia chemba ya pua na kinywa.
a)Irabu b)Konsonanti c)Silabi d)Fonimu ( )

2. Oanisha dhana za orodha A na maelezo ya Orodha B kwa kuandika herufi ya orodha B mbele ya namba ya orodha A

ORODHA A	ORODHA B
i) Vitenzi……..	a) Maneno yanayofafanua zaidi juu ya vitenzi
ii) Nomino……	b) Maneno yanayodokeza vionjo vya moyo
iii) Viwakilishi…….	c)Maneno yanayotaja tendo
iv).Vielezi……	d)Maneno yanayounganisha dhana moja na nyingine
v).Vihisishi……..	e) Maneno yanayotaja majina ya vitu,watu au mahali
	f) Maneno yanayosimama badala ya nomino
	g)Maneno yanayoonesha uhusiano uliopo baina ya vitu

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii na utoe majibu mafupi

3..Misimu ni nini? Eleza kwa kifupi aina tatu za misimu

4. Onesha dhima nne za lahaja

5. Unda vitenzi viwili kwa kila nomino zifuatazo;
i) Mchezo ii) Azimio iii) Wito iv) Matapishi

6. Tenga kiima (k) na kiarifu (k)katika sentensi zifuatazo;
i)Mwalimu wetu alitaka kutufundisha wakati wa jioni
ii)Huyu si mwenzetu
iii) Wale waliotukebehi juzi nimewaona wakitapatapa njiani
iv) Sisi huwa tunapenda kula ugali lakini wao wanapenda kula chips

7. Fafanua kwa ufupi dhana zifuatazo za kifasihi huku ukionesha mifano
a)Tasfida b) Mubaalagha c)Tashihisi d)Tashititi
d) Mjalizo e) Tashibiha f) Sitiari g)Onamatopeia

8. Soma kifungu cha habari kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:-

Aaa! Maskini ya Rabi eee! Hii ndiyo nchi tuliyomo sisi! Nchi inayovuja jasho! Nchi omba omba, nchi maskini, nchi ambayo wanawake huvaa nguo …… ! Nchi ambayo wanawake huvaa nywele za maiti ……. Nchi ambayo wasichana wake hawautaki Uafrika ……. haya ndiyo maendeleo yetu ……

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

Haki na usawa katika nchi maskini ni ndoto. Wengi huamua kuwa mabubu mara tu demokrasia inapopokonywa na watu wachache. Huu ni unafiki mkubwa. Haki haipo nchini mwetu ila tu tumefumbwa macho. Tumekuwa vipofu.

Mimi nimeamua kupambana. Nitachukua pinde …….. Nitachkuwa sime …….. nitachukua mkuki …….. Nitachukua upinde …….. Nitachukua mishale …….. nitapigana kufa na kupona. Nitapigania haki na usawa. Haki! Haki! Usawa! Haki! Haki ……. maana yake ni nini?

MASWALI

(a) Taja maudhui ya habari hii kwa neno moja na kwa herufi kubwa
(b) Je,hatua anazochukua mhusika katika aya ya tatu zinaweza kuleta madhara gani kwa jamii.?
(c) Nywele za maiti zinazozungumzwa katika aya ya kwanza ni nywele za namna gani?
(d) Fafanua funzo moja unalolipata katika matini hii kuhusu njia sahihi ya kudai haki.

SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswali matatu tu katika sehemu hii na utoe maelezo ya kina

ORODHA YA VITABU TEULE

USHAIRI/ DIWANI

1. Wasakatonge……m.s Khatibu (DUP)
2. Malenga wapya……TAKILUKI (DUP)
3. Mashairi ya cheka cheka…….TA Mvungi (E.P and D.LTD

RIWAYA

1. Takadini……..Ben Henson (mbs)
2. Watoto wa mama ntilie……..E. Mbogo (HP)
3. Joka la mdimu……A.J.safari (HP)

TAMTHILIYA

1. Orodha……Steve Reynolds (MA)
2. Ngoswe kitovu cha uzembe……E. Semzaba (ESC)

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

3. Kilio chetu……..Medical Aid Foundation

9. Chukulia kuwa wewe ni Elizabeth fidelis ambaye ni mkuu wa mkoa wa Morogoro.Siku za hivi karibuni mkoa wa morogoro umegubikwa na migogoro mingi baina ya wakulima na wafugaji .Andika hotuba utakayowasomea wananchi wako wa mkoa wa Morogoro .Hotuba yako ijikite katika kukemea migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

10.Watunzi wa kazi za fasihi daima huandika yale wanayoyaona katika jamii.Thibitisha madai haya kwa hoja tatu kutoka katika kila diwani mbili ulizosoma

11.Waandishi wa kazi za fasihi humtazama mwanaume katika mitazamo ya namna mbili(hasi na chanya) .Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma onesha namna waandishi walivyomtazama mwanaume kwa mtazamo hasi.Toa hoja tatu kwa kila kitabu.

12 a) Majigambo ni nini?

b)Chukulia kuwa wewe ni askari .Umeteuliwa kutamba majigambo katika sherehe za siku ya mashujaa.Andika majigambo yenye beti tatu utakayotamba katika sherehe hiyo.

----------TAMATI----------

Search ⇢ www.africona.net